

UTUPAJI MIMBA KWA NG'OMBE (ABORTION IN CATTLE)

Na Augustino Chengula

Utangulizi

Kutupa mimba ni kitendo cha kutolewa kwa ndama wa ng'ombe nje ya mfuko wa uzazi na mara nyingi akiwa amekufa kunakotokea kati ya siku ya 42 hadi siku takribani ya 260 kabla ya siku zake za kuzaa kawaida. Mimba yeyote inayopotea kabla ya siku ya 42 inajulikana kama “**kifo kiinitete**” (embryonic death) na kile kinachotokea kati ya siku 260 na muda wa kawaida wa kuzaa hujulikana kama “**ndama asiye riziki**” (stillbirth). Kutupa mimba isiyozidi mitano kwa kila ng'ombe 100 kwa mwaka huonekana kitu cha kawaida katika shamba, ingawa kila upotevu wa ndama mmoja katika hatua yeyote ile una maana kubwa sana kwa upande wa kipato wa mfugaji.

Visababishi vya utupaji wa mimba

Utupaji wa mimba kwa ng'ombe unaweza kusababishwa na vitu vingi sana na vimegawanyika katika makundi mawili makubwa ambayo ni vitu visivyo na maambukizi na vile vyenye maambukizi. Vitu visivyo na maambukizi ni kama kukosekana kwa usawa wa homoni mwilini, hitilafu ya vinasaba, mabadiliko ya kimazingira kama kuongezeka kwa joto kunakomsababishia msongo (au usumbufu) na sumu ya vyakula mfano inayotokana na fangasi.

Vitu vyenye maambuki ni vimelea vya magonjwa yanayosababisha homa kali, wanaweza kuwa bakteria, virusi protozoa, au fangasi. Kielelezo hapa chini kinaonyesha ugonjwa na aina ya mdudu anayesababisha ugonjwa pamoja na umri wa mimba anao athiri.

Magonjwa yanayosababishwa na vimelea aina ya protozoa						
Ugonjwa na jina la Kimelea	Ueneaji	Idadi ya wanatupa mimba	Umri wa mimba inayotupwa	Aina ya chanjo	Sampuli ya kukusanya	Ushauri au Upambanaji
Homa ya kutupa mimba (Brucellosis) (<i>Brucella abortus</i>)	Kupitia mkojo, mimba iliyotupwa, na maji yenye wadudu (mkojo)	Hadi 80% ya ng'ombe wasio chanjwa	Miezi 6-9	Chanjo hai (Live vaccine) kwa mitamba	Kondo la nyuma, ndama aliyekufa, na damu ya aliyetupa mimba na ng'ombe wengine	Dume wasichanjwe, wenye ugonjwa waondolewe shambani
Leptospirosis	Kupitia mkojo,			Chanjo		Sampuli maabara

<i>(Leptospira interrogans)</i>	mimba iliyotupwa, na maji yenye wadudu (mkojo)	5-40%	Miezi 6-9	mfu(Killed vaccine) hukinga kwa miezi 6	Kondo la nyuma, ndama aliyekufa, na damu	kujua kisababishi
Vibriosis <i>(Campylobacter fetus venerealis)</i>	Madume yenye ugonjwa, na kula vyakula vyenye wadudu	Zaidi ya 10%	Miezi 4-8	Chanjo mfu	Maosheo ya uzazi wa dume, kimiminika sehemu ya uzazi wa jike, ndama na kondo la nyuma	Madume hubeba ugonjwa, Majike huonekana kama yana shida ya kuzaa (ugumba)
Listeriosis <i>(Listeria monocytogenes)</i>	Husambazwa panya, na majani yaliyovunda	Hutokea mara moja moja na hufikia 40%	Muda wowote, zadi muda karibu na kuzaa	Haipo	Kondo la nyuma, ndama aliyekufa, na damu ya aliyetupa mimba	
Magonjwa yanayosababishwa na vimelea aina ya protozoa						


Trichomoniasis (<i>Tritrichomonas foetus</i>)	Huenezwa na ng'ombe dume	Hutokea mara mojamoja	Miezi 2-4	Chanjo mfu	Nyumba ya uzazi, sehemu ya mbele ya sehemu ya uzazi ya dume	Ondoa madume yote na majike yasiyozaa, pumzisha dume kupanda kwa siku 60-90
Magonjwa yanayosababishwa na vimelea aina ya Fangasi						
<i>Aspergillus sp</i> (60-80%) <i>Mucor sp, Absidia, or Rhizopus sp</i>	Kwa kula vyakula vyenye fangasi	Hutokea mara moja moja na huwa kati ya 5-10%	Miezi 4-9 hasa wakati wa baridi	Haipo	Kondo la nyuma na ndama aliyekufa	Husababisha 3-10% ya mimba zote zinazotupwa
Magonjwa yanayosababishwa na vimelea aina ya Fangasi						
Ugonjwa wa kuharisha (Bovine)	Maambukizi toka ng'ombe mmoja	Kwa kawaida huwa chini	Inabadilika, kawaida	Chanjo hai au mfu	Damu mara mbili tofauti ya wiki 3,	Wachanje wakiwa na miezi 8

Viral Diarrhoea Virus- BVDV)	kwenda mwingine		mapema hadi miezi 4		ndama, kondo la nyuma	
Pua nyekundu [nfectious Bovine rhinotracheitis virus (IBRV)]	Toka kwa ng'ombe jike mwenye ugonjwa	5-60 kwa ng'ombe ambao hawakuchanjwa	Miezi 4-9	Chanjo hai au mfu	Damu, ndama, kondo la nyuma	Tumia chanjo mfu kwa ng'ombe wenye mimba
NB: Yapo magonjwa mengi yanayoweza kusabisha mimba ipotee, lakini haya ni ya muhimu kuyaangalia kwa karibu kwani yanachangia kwa kiasi kikubwa.						

Mwongozo wa kutambua umri wa mimba iliyopotea (makadirio)

Umri wa mimba (Miezi)	Maelezo yahasuyo ndama mwenyewe
2	Ukubwa kama panya wadogo (mouse)
3	Ukubwa kama panya wakubwa (rat)
4	Ukubwa kama paka mdogo

- 5 Ukubwa kama paka mkubwa
 - 6 Ukubwa kama mbwa mdogo (ana nywele kuzunguka macho, pua, mdomo na mkia)
 - 7 Ana nywele laini mwilini na miguuni
 - 8 Ana nywele mwili mzima, meno ya kukatia yameenza kujitokeza
 - 9 Meno ya kukatia yameshaota tayari
-



Jinsi ya kuzuia utupaji wa mimba kwa ng'ombe

1. Hakikisha mahali wanapolala ng'ombe ni pasafi siku zote na kwa wale wanaokamuliwa maeneo ya ukamujaji yawe safi.
2. Hakikisha unatumia madume yaliyoidhinishwa kuwa hayana magonjwa au chukua kwenye shamba lenye uhakika wa kutokuwa na magonjwa ya kutupa mimba

3. Hakikisha majike yenye ugonjwa yanatengwa na kuondolewa mara moja kwenye shamba lako ili yasisambaze ugonjwa
4. Ndama waliotolewa, kondo la nyuma na vitu vingine vinavyoendana na kutupwa mimba viondolewe mara moja na kufukiwa kiasi ambacho mbwa au wanyama wengine hawawezi kufukua
5. Chakula kwa ajili ya ng'ombe kiwe kimehakikiwa uwepo wa fangasi au kinunuliwe kwa wauzaji wa uhakika
6. Chanja wanyama wako dhidi ya magonjwa yanayopelekea upotezaji wa mimba, pata ushauri kwa mtaalamu wa mifugo wakati unaofaa kuchanja mifugo yako.
7. Weka kumbukumbu za uzaaji vizuri ili usiwape dawa zitakazo sababisha utokaji wa mimba, lakini pia kujua mapema ng'ombe yupi anashida ya uzazi.

MAREJEO

1. Belinda Walker, 2005. Diseases causing reproductive losses in breeding cattle, Veterinary Officer, Gunnedah
2. Clell V. Bagley, 1999. ABORTION IN CATTLE, Extension Veterinarian, Utah State University, Logan UT 84322-5600
3. Michael Yaeger, 1993. Cattle Abortions - Causes and Prevention, South Dakota State University, Brookings, SD

4. Ernest Hovingh, 2009. Abortions in Dairy Cattle – I Common Causes of Abortions, Extension Veterinarian, Virginia-Maryland Regional College of Veterinary Medicine, Virginia Tech
5. Ernest Hovingh, 2009. Abortions in Dairy Cattle – II Diagnosing and Preventing Abortion Problems, Extension Veterinarian, Virginia-Maryland Regional College of Veterinary Medicine, Virginia Tech
6. Dr. R.A. Dailey, Abortion in Dairy Cows and Heifers, West Virginia University
7. Anima Health and Veterinary laboratory Agency, 2012. Abortion in cattle, http://vla.defra.gov.uk/reports/rep_papers.htm
8. Guy E. Reynolds, 1914. Infectious Abortions in Cattle, Revised and updated by Stuart D. Lincoln, Department of Veterinary Science, Caine Veterinary Teaching and Research Center, Caldwell, University of Idaho